Ripoti Ya Uwajibikaji

Serikali Kuu

2015-16

Ripoti Ya Uwajibikaji

Serikali Kuu

2015-16

Kwa kushirikiana na:

Kwa msaada wa:

Mradi wa Good Financial Governance (GFG)

Unaotekelezwa na:

Kwa niaba ya:

Co-funded by European Union

Swiss Agency for Development and Cooperation SDC

Yaliyomo

Orodha ya Vielelezo ii
Vifupisho iii
Utangulizi iv
Hati za Ukaguzi 1
Aina ya Hati zitolewazo na CAG 1
Mwenendo wa hati za ukaguzi na mapendekezo ya CAG 1
Mwenendo wa Utekelezaji wa mapendekezo ya CAG 2
Masuala Muhimu yaliyojitokeza katika Ukaguzi wa 2015/2016 4
Jambo la 1: Deni La Taifa 4
Jambo la 2: Matumizi Mabaya ya Misamaha ya Kodi 6
Jambo la 3: Makadirio ya kodi ambayo hayajakusanywa Sh. 588.83 bilioni 7
Jambo la 4: Upungufu wa mashine za EFD asilimia 84. 7
Jambo la 5: Udhibiti wa Ndani na Utawala bora 8
Jambo la 6: Usimamizi wa Rasilimali Watu na Mishahara 9
Jambo la 7: Upungufu wa Watumishi 11
Jambo la 8: Utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma 2011 12
Jambo la 9: Ukaguzi wa Vyama vya Siasa 13
Jambo la 10: Ukaguzi Maalum wa Fedha za Gavi Alliance Kwa Ajili ya Chanjo ya Surua Rubella 14
Hitimisho 14

Orodha ya Vielelezo

Kielelezo Na. 1: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Serikali Kuu mwaka 2013/14 hadi 2015/16 2

Kielelezo Na. 2: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2015/16.....2

Kielelezo Na. 3: Mgawanyo wa Kodi ambazo hazijakusanywa kwa Idara za ukusanyaji kodi 7

Kielelezo Na. 4: Idadi ya wafanya biashara wanaotakiwa kuwa na mashine za EFD na idadi ya wafanya biashara ambao hawana mashine za EFD..... 8

Kielelezo Na. 5: Wizara na Sekretariati za Mikoa zinazoongoza kwa Uhaba wa Watumishi.....11

Vifupisho

CAG	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
WAJIBU	Taasisi ya Uwajibikaji Kwa Umma
NBAA	Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu
IPSASs	Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Taasisi za Umma
PAC	Kamati ya Kudumu ya Usimamizi ya Bunge inayoshughulikia Hesabu za Serikali Kuu
CCK	Chama Cha Kijamii
AFP	Tanzania Farmers Party
NLD	National League for Democracy
VAT	Kodi ya Ongezeko la Thamani
EFD	Mashine ya Kielekroniki ya kukusanya Mapato
IAG	Mkaguzi Mkuu wa Ndani
NRA	National Reconstruction Alliance
UPDP	United Peoples' Democratic Party
CHAUMMA	Chama cha Ukombozi wa Umma
UMD	Union for Multi party Democracy

Utangulizi

Taasisi ya WAJIBU ni taasisi fikra ya uwajibikaji wa Umma iliyoanzishwa mwaka 2015 kwa lengo la kutengeneza mazingira ya kukuza uwajibikaji na Utawala bora hapa nchini. Ili kukamilisha adhma hiyo, WAJIBU kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2015/16 ya Serikali Kuu imeandaa Ripoti ya Uwajibikaji katika Serikali Kuu. Serikali Kuu kisheria inajumuisha Wizara, Wakala, Idara za Serikali, Sekretarieti za Mikoa pamoja na Ofisi za Ubalozi wa Tanzania zilizo nje ya Tanzania. Ripoti hii ni majumuisho ya masuala yaliyoibuliwa na CAG kwa mwaka 2015/16 katika ukaguzi wa Taasisi 222 sawa na asilimia 88 ya taasisi 253 zilizotakiwa kukaguliwa. Taasisi 31 sawa na asilimia 12 ya taasisi zilizotakiwa kukaguliwa hazikuweza kukaguliwa kwasababu ya ukosefu wa fedha na sababu nyinginezo. Katika mwaka 2015/16 bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilipunguzwa kwa asilimia 40.

Katika Kuandaa ripoti hii ya kwanza ya uwajibikaji WAJIBU, imeshirikiana na GIZ ambayo ni taasisi ya utekelezaji ya Ushirikiano wa Ujerumani Tanzania kupitia mradi wa Utawala bora wa Fedha za Umma (Good Financial Governance). Mradi huu unatekelezwa na GIZ kwa niaba ya Umoja wa Ulaya, Ushirikiano wa Ujerumani Tanzania, na Shirika la Maendeleo la Uswisi. Ripoti hii itakuwa inatolewa kila mwaka na itakuwa katika lugha rahisi na rafiki kwa ajili ya wananchi wa kawaida. Pia, ripoti hii itachambua mapendekezo ya CAG yaliyotolewa kutokana na ukaguzi wa Serikali Kuu yenye umuhimu mkubwa kwa Umma.

WAJIBU inatarajia ripoti hii itaongeza uelewa wa wananchi juu ya ripoti ya CAG ya Serikali Kuu ya mwaka 2015/16. Pia, WAJIBU inatarajia ripoti hii itawawezesha wananchi kudai uwajibikaji kutoka kwa watendaji wa Serikali pale watakapoona hawajawajibika ipasavyo. Vilevile, ripoti hii itafanya mapendekezo ya CAG yawe na uhai wa muda mrefu zaidi kuliko ilivyokuwa huko nyuma, hivyo itachangia kuongeza utekelezaji wa mapendekezo hayo.

Ripoti hii imegawanyika katika sehemu Sita (6), Sehemu ya kwanza ni Utangulizi, sehemu ya pili ni Hati za Ukaguzi, sehemu ya tatu ni Utekelezaji wa Mapendekezo ya miaka ya nyuma, sehemu ya nne ni utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Usimamizi ya Bunge inayoshughulikia Hesabu za Serikali Kuu (PAC), sehemu ya tano ni Masuala Muhimu yaliyojitokeza katika Ukaguzi wa mwaka 2015/16 na sehemu ya sita ni hitimisho.

Ludovick S. L. Utouh

Mkurugenzi Mtendaji

WAJIBU – Institute of Public Accountability

Hati za Ukaguzi

Hati za Ukaguzi ni maoni ya Mkaguzi wa Hesabu kuhusu hesabu za Taasisi inayokaguliwa. Maoni haya yanaonesha kama hesabu zilizokaguliwa zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya kihasibu vya kimataifa (IPSASs) na matamko yanayotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA).

Aina ya Hati zitolewazo na CAG

Katika ukaguzi wa Serikali Kuu, wakaguzi hutoa hati zifuatazo;

i. **Hati inayoridhisha (hati safi):** Hati hii inatolewa wakati Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu za mkaguliwa zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu (International Accounting Standards), na vile vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA).

ii. **Hati Yenye Mashaka:** Aina hii ya hati hutolewa pale mkaguzi anapokutana na mazingira ya kuwepo kwa makosa ya msingi ya kiuhasibu yanayohusu mapato, matumizi au rasilimali ya taasisi inayokaguliwa.

iii. **Hati Isiyoridhisha:** Hati isiyoridhisha inatolewa pale Mkaguzi anapoona kuwa, taarifa za fedha na rasilimali za mkaguliwa kwa kiasi kikubwa zina makosa ya msingi ya kiuhasibu na kiutendaji pamoja na kuwepo na usimamizi mbovu wa mifumo ya udhibiti ya ndani.

iv. **Kushindwa kutoa Hati (Hati Mbaya):** Hali hii kulingana na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndiyo inayozungumziwa kama, Hati mbaya Ya ukaguzi Taarifa ya aina hii hutolewa pale ambapo mkaguzi anajiridhisha kuwa mkaguliwa hana kumbukumbu za fedha na rasilimali zinazotoshelesha kutengeneza taarifa za mahesabu ya taasisi pamoja na kuwepo udhaifu mkubwa wa usimamizi wa mifumo ya udhibiti ya ndani.

Katika ukaguzi wa Serikali Kuu, endapo taasisi itapata hati isiyoridhisha au hati mbaya, hakuna athari za moja kwa moja katika rasilimali zinazoweza kupatikana. Aina hii ya hati hutia shaka usahihi wa taarifa za mapato na matumizi ya rasilimali za taasisi husika. Hata hivyo, WAJIBU inashauri serikali kuutekeleza utaratibu uliopo wa kuwachukulia hatua watendaji wa taasisi zitakazopata aina hizo za hati.

Mwenendo Wa Hati Za Ukaguzi Na Mapendekezo Ya CAG

Kwa mwaka 2015/16, ripoti ya CAG inaonesha kuwa kati ya Taasisi 222 ambazo ni Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Serikali za mikoa zilizokaguliwa, Taasisi 190 sawa na asilimia 86 zilipata Hati Zinazoridhisha; Taasisi 24 sawa na asilimia 11 zilipata Hati Zenye Shaka, Taasisi 3 sawa na asilimia 1 zilipata Hati Zisizoridhisha na Taasisi 5 sawa na asilimia 2 zilipata Hati Mbaya. Hati Mbaya zilitolewa kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Chama cha AFP, Chama Cha Kijamii (CCK), Chama cha toa mabano na Chama cha Sauti ya Umma ya Umma (Kujua aina ya hati zilizopatikana katika Taasisi nyingine pitia ripoti ya CAG ya Serikali Kuu ya mwaka 2015/16 inayopatikana katika tovuti ya http://www.nao.go.tz). Kadhalika, mwenendo wa hati za ukaguzi kwa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Serikali za mikoa kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita ni kama ilivyooneshwa katika Kielelezo Na.1 hapo chini.

Kielelezo Na. 1: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Serikali Kuu mwaka 2013/14 hadi 2015/16



Mwenendo wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya CAG

Katika mwaka 2014/15 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alitoa jumla ya mapendekezo 102 katika ukaguzi wa Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Sekretariati za Mikoa. Kati ya hayo, mapendekezo 19 sawa na asilimia 18.6 yalitekelezwa kikamilifu, mapendekezo 53 sawa na asilimia 52 yapo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji, mapendekezo 20 sawa na asilimia 19.6 hayajatekelezwa na mapendekezo 10 sawa na asilimia 9.8 hayajatekelezwa kabisa kwa kuwa yamepitwa na wakati. Kwa ujumla, utekelezaji wa mapendekezo hayo ni wa wastani kama inavyooneshwa kwenye kielelezo Na. 2 hapo chini:

Kielelezo Na. 2: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2015/16



Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Usimamizi ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC)

Katika ripoti za ukaguzi za taasisi moja moja, Kamati ya Kudumu ya Usimamizi ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ilitoa maelekezo 290 ambayo yalihitaji utekelezaji wa Serikali kupitia kwa Maofisa Masuuli wa taasisi husika.

Hata hivyo, Kamati ya Kudumu ya Usimamizi ya Bunge ya Hesabu za Serikali iliweza kupitia ripoti za Wizara, Idara, Balozi, Wakala na Sekretariati za Mikoa 49 tu kati ya ripoti 199 zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hii ni sawa na asilimia 25 tu ya ripoti zote zilizotolewa.

Athari: Hali hii inaonesha kuwepo kwa ufanisi usioridhisha wa PAC katika kusimamia taasisi za Serikali. Kutokana na hali hiyo, Bunge linakosa takribani asilimia 75 ya taarifa za utendaji kazi wa Serikali Kuu hivyo kushindwa kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia Serikali ipasavyo.

Mapendekezo:

1. Serikali ione umuhimu wa kuziongezea muda na fedha za uendeshaji Kamati za Kudumu za Usimamizi za Bunge. Hii itaziwezesha Kamati hizo kupitia ripoti nyingi zaidi, hivyo kuliwezesha Bunge kusimamia utendaji kazi wa Serikali vizuri zaidi.
2. Asasi za kiraia zione namna zinavyoweza kufanya uchambuzi wa taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na kuongeza taarifa za kisekta kwa Kamati za Bunge. Zipo Asasi nyingi zenye taarifa za kutosha juu ya usimamizi wa fedha na rasilimali za umma kama vile Sikika kwenye sekta ya afya, Haki Elimu kwenye sekta ya elimu n.k. Kama taarifa hizi zitafikishwa kwa kamati za Bunge zitasaidia kurahisisha utendaji kazi wa kamati hizo.
3. Jukumu la PAC limekuwa kubwa sana baada ya kupewa jukumu la usimamizi wa Mashirika ya Umma. Hivyo, kuna umuhimu wa Bunge kuona aidha uwezekano wa kuunda kamati pacha ya

kushughulikia usimamizi wa mashirika ya umma au kuweka muundo maalum wa kamati hii ili imudu ukubwa wa kazi iliyo mbele yake.

Mambo Muhimu Yaliyojitokeza Katika Ukaguzi wa 2015/16

Katika ukaguzi wa mwaka 2015/16, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ametoa mapendekezo ya ujumla 12 kwa Serikali kuu. Mapendekezo hayo yalitokana na mambo mbalimbali yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa hesabu za Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Idara, Ofisi za Balozi, Wakala wa Serikali pamoja na Kaguzi Maalum. Mambo yaliyobainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yenye umuhimu mkubwa kwa maslahi ya taifa, athari na mapendekezo yake ni kama ifuatavyo:

Jambo la 1: Deni la Taifa

Kufikia tarehe 30 Juni, 2016, deni la Taifa lilikuwa shilingi trilioni 41.04 ambapo deni la ndani lilikuwa shilingi trilioni 11.20 sawa na asilimia 27 na deni la nje trilioni 29.84 sawa na asilimia 73. Deni hili limeongezeka kwa shilingi trilioni 7.50 sawa na asilimia 22 ikilinganishwa na deni la shilingi trilioni 33.54 lililoripotiwa tarehe 30 Juni, 2015. Deni hili halihusishi madeni yafuatayo:

- Madeni ya huduma na bidhaa ambazo serikali ilitumia na haijalipa,
- Madeni ya wafanyakazi wa serikali,
- Madeni ya mikataba ya ujenzi na huduma mbalimbali,
- Baadhi ya madeni/mikopo ya mifuko ya hifadhi ya jamii (Pension Funds), na
- Madeni ya ndani ya moja kwa moja kwenye Mashirika ya Umma na Serikali za Mitaa

Mapungufu yaliyobainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwenye deni la Taifa ni kama ifuatavyo:

- Kuongezeka kwa gharama za kuhudumia deni la taifa kulikosababishwa na ongezeko la mikopo isiyo ya masharti nafuu kutoka asilimia 11 mwaka 2011/12 mpaka asilimia 31 ya deni la nje kufikia tarehe 30 Juni, 2016.
- Kutoingizwa kwenye vitabu vya Serikali kwa kiwango cha deni la taifa cha kiasi cha shilingi trilioni 3.22. Kiasi hicho kimetokana na madeni ya mifuko ya pensheni yaliyohakikiwa kiasi cha shilingi trilioni 2.99 na dhamana zilizokiukwa masharti kiasi cha shilingi bilioni 225.6.
- Serikali ilipanga kukopa kupitia hati fungani kugharamia Bajeti kiasi cha Shilingi 2.6 trilioni, hata hivyo Serikali ilikopa kiasi cha Shilingi 4.48 trilioni sawa na asilimia 42 zaidi ya kiwango kilichopangwa.

Athari

1. Mzigo mkubwa kwa Serikali kuhudumia deni la taifa kunaipunguzia Serikali uwezo wa fedha za kushughulikia upatikanaji wa huduma bora za jamii kama vile afya, maji pamoja na shughuli nyingine za maendeleo. Mfano; katika bajeti ya mwaka 2015/16, bajeti iliyotengwa kuhudumia deni la taifa ilikuwa ni Shilingi trilioni 6.40 wakati kiasi kilichotengwa kugharamia miradi yote ya maendeleo nchini kilikuwa ni Shilingi trilioni 5.92 (Chanzo: Government budget for financial year 2015/16 citizens' budget edition –issued by Ministry of Finance and Planning in collaboration with Policy Forum).

2. Ingawaje ukubwa wa deni la taifa bado upo kwenye uwiano unaokubalika kwa kutumia vigezo vya Benki ya Dunia, tahadhari ni lazima itolewe kuhusu mambo mawilli yafuatayo:

    i. Ukopaji wa Serikali ulenge katika kuwekeza kwenye vitega uchumi vya nchi vitakavyochangia ukuaji wa uchumi wa nchi na hivyo kuchangia katika kujenga uwezo wa nchi kulipa madeni yake mara yatakapoiva.

    ii. Mikopo inayokopwa ni kwa fedha za kigeni, na malipo yake yatakuwa kwa fedha za kigeni, hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kuchunga thamani ya fedha zetu isishuke mno kwa kuwa kwa kufanya hivyo Serikali itakuja kuhitaji fedha nyingi za ndani kulipia madeni yake ya nje.

Pendekezo

1. Ni wakati sasa kwa asasi za kiraia na taasisi zingine zisizo za kiserikali kuanza kudai uwazi zaidi wa matumizi ya fedha za mikopo.

2. Bunge kama mwakilishi wa wananchi lishirikishwe kwenye mikopo mikubwa ya kitaifa. Pia Bunge liisisitizie Serikali kufanya yafuatayo;

   a) Kupitia Mkakati wa Taifa wa Madeni, Kuhakikisha Sera ya usimamizi wa Deni la Taifa inazingatiwa, na

   b) Kuharakisha marekebisho ya Sheria ya Mikopo, Dhamana, na Misaada ya mwaka 1974 (kama ilivyorekebishwa 2004) na kanuni zake za 2003 ili kukabiliana na changamoto zilizopo katika usimamizi wa Deni la Taifa.

Jambo la 2: Matumizi Mabaya ya Misamaha ya Kodi

Pamoja na serikali kutoa misamaha ya kodi kwa sababu mbalimbali, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alibaini mapungufu kadhaa katika usimamizi wa matumizi ya misamaha hiyo ya kodi. Katika ripoti ya mwaka 2015/16 yalibainika mapungufu mbalimbali yakiwemo;

a) Misamaha ya kodi kiasi cha shilingi trillion 1.1

Taarifa za Fedha za Mamlaka ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2015/16 zinaonesha serikali ilitoa misamaha ya kodi yenye thamani ya shilingi trilioni 1.10 sawa na asilimia 1.14 ya pato la ndani la taifa kwa mwaka 2015/16. Kiasi hiki ni kikubwa ukilinganisha na lengo la serikali kupunguza misamaha ya kodi hadi kufikia chini ya asilimia 1 ya pato la ndani la taifa kwa mwaka.

b) Misamaha ya Kodi kuwanufaisha watu wasiostahili shilingi billioni 3.46

Kwa kipindi cha mwaka 2012 hadi 2014 magari 238 kutoka nje ya nchi yaliingizwa nchini kwa kutumia majina ya walipakodi wawili (M/s Lake Trans Ltd na M/s State Oil (T) Ltd) ambao walipewa misamaha ya kodi katika uingizaji wa magari hayo. Baada ya ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ilibainika kuwa magari hayo yalimilikiwa na watu tofauti ambao hawakustahili kunufaika na misamaha ya kodi ya magari hayo.

c) Kutumia misamaha ya kodi ya mafuta ya uchimbaji wa madini kwa kampuni zisizohusika na uchimbaji wa madini

Katika uchambuzi wa nyaraka za matumizi ya mafuta yaliyopewa misamaha ya kodi katika kampuni ya uchimbaji wa madini ya dhahabu ya Buzwagi, iligundulika kuwa lita 20,791,072 za mafuta katika kipindi cha miezi 18 kuanzia mwezi Julai, 2014 hadi Disemba, 2015 yalikuwa yamesafirishwa kwenda kwa mkandarasi M/S Aggreko Company Ltd ambaye hakustahili kupewa msamaha wa kodi.

Athari: Misamaha ya kodi inaikosesha serikali vyanzo vya mapato yake ya ndani ambayo yangesaidia kupata pesa za kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo hivyo kuathiri maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja.

Pendekezo:

i. Serikali iongeze uwazi katika misamaha ya kodi inayotolewa, hii ni pamoja na asasi za kiraia kuipitia ripoti maalumu ya misamaha ya kodi inayotolewa kwa kila robo mwaka. Taarifa hii inapatikana kupitia tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango.

ii. Serikali ije na sera madhubuti ya utoaji wa misamaha ya kodi ambapo sera hii itaonesha wazi

ni ofisi zipi na maafisa wapi watakaokuwa wanashughulikia utoaji wa misamaha hiyo. Sera hiyo itamke wazi madaraka ya maofisa mbalimbali katika utoaji wa misamaha ya kodi pamoja na namna ya ukokotoaji wa misamaha ya kodi.

Jambo la 3: Makadirio ya Kodi ambayo Hayajakusanywa Sh. 588.83 Bilioni

Rejista inayohifadhi taarifa za kodi ambazo hazijalipwa pamoja na nyaraka mbalimbali zimeonesha kuwa kiasi cha kodi cha shilingi 588.8 billioni hazikukusanywa kutoka kwa walipa kodi mbali mbali. Katika kiasi hicho, jumla ya shilingi 71.0 bilioni kinatokana na Idara ya Walipa Kodi Wakubwa. Kiasi cha shilingi 92.0 bilioni kinahusiana na Idara ya Uchunguzi wa Kodi. Na, kiasi cha shilingi 425.8 bilioni kinahusiana na Idara ya Mapato ya Ndani katika mikoa 10 ya kodi.

Kielelezo Na. 3: Mgawanyo wa Kodi ambazo hazijakusanywa kwa Idara za ukusanyaji kodi



Athari: Kutokukusanywa kwa kodi kunarudisha nyuma juhudi za Serikali katika kuleta maendeleo kwa taifa.

Mapendekezo:

Asasi za Kiraia na wadau wengine kuisisitizia Serikali na Bunge kupitia upya mfumo wa kodi na kufanya mabadiliko ya kuuboresha ili kupunguza tatizo la ukwepaji wa kodi. Mfano, kupunguza mamlaka ama vituo ambavyo biashara au mtu moja atatakiwa kwenda kulipa kodi, hii ni pamoja na idadi ya kodi atazotakiwa kulipa.

Jambo la 4: Upungufu wa Mashine za EFD Asilimia 84

Katika uchunguzi uliofanyika kwa kipindi cha mwezi Julai, 2015 hadi Novemba, 2016 ilibainika kuwa

i. Katika walipa kodi waliosajiliwa kukusanya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) 9,743, ni walipa kodi 1,578 ambao ni asilimia 16 tu ndio wanatumia mashine za EFD na walipa kodi 8,165 ambao ni sawa na asilimia 84 hawakuwa na mashine za EFD.

ii. Kadhalika, kati ya walipa kodi 49,009 wanaostahili kutumia mashine za EFD kukusanya

Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), ni walipa kodi 9,127 ambao ni asilimia 18.6 tu ndio wenye mashine hizo wakati walipa kodi 39,882 ambao ni sawa na asilimia 81.4 hawakuwa na mashine hizo.

Kielelezo Na. 4: Idadi ya wafanya biashara wanaotakiwa kuwa na mashine za EFD na idadi ya wafanya biashara ambao hawana mashine za EFD



Athari: Upotevu wa Kiasi kikubwa cha mapato ya Serikali kupitia kodi ya ongezeko la thamani kutokana na Mamlaka ya Mapato kutokuwa na uhakika wa kiasi cha mauzo ya wafanyabiashara.

Pendekezo: Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato waongeze usambazaji wa mashine za EFD. Pia, Asasi za kiraia na taasisi mbalimbali zisisitize utumiaji wa mashine za EFD kwa kuhakikisha wananchi hawanunui kutoka kwa mfanyabiashara asiye na mashine ya EFD.

Jambo la 5: Udhibiti wa Ndani na Utawala Bora

Udhibiti wa ndani ni mchakato wa kuhakikisha malengo ya taasisi yanafikiwa, hii ikijumuisha: uwepo wa ufanisi, uzingatiaji wa sheria, kanuni na sera katika kulinda mali na kuwa na taarifa sahihi za kihasibu. Wakaguzi wa ndani wana wajibu mkubwa wa kupitia na kuthibitisha kama taasisi inazingatia sheria, kanuni, sera na taratibu zilizowekwa. Maafisa Masuuli, Bodi za Ushauri (Managerial Advisory Board), menejimenti za taasisi na wafanyakazi wengine wana jukumu la kuhakikisha kuwa mifumo ya udhibiti ya ndani inafanya kazi kama inavyopaswa.

a. Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

Tathmini ya ukaguzi iliyofanyika kuhusu vitengo vya ukaguzi wa ndani kwenye sampuli ya Wizara, Sekretariati za Mikoa, Idara, Wakala na Taasisi nyingine za serikali, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alibani kuwa Taasisi 33 zikijumuisha Wizara na Idara 14, Sekretarieti za Mikoa 17 na Taasisi zingine 2 kuwa na mapungufu kama vile kutokuanzishwa kwa vitengo vya ukaguzi wa ndani, vitendea kazi hafifu na mipango ya ukaguzi wa ndani kutoidhinishwa na Kamati ya Ukaguzi.

b. Kamati ya Ukaguzi

Katika tathmini ya ukaguzi wa utendaji wa Kamati za Ukaguzi katika Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa na Wakala wa serikali, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alibaini Taasisi 31 zikijumuisha Wizara na Idara 14, Sekretarieti za Mikoa 12 na Taasisi zingine 5 zilipatikana na mapungufu mbalimbali ikiwa ni pamoja na; Taasisi kutokuwa na Kamati ya Ukaguzi, kutokujadili na kuidhinisha mpango mkakati wa mwaka wa ukaguzi wa ndani na kutokupitia taarifa za hesabu za Taasisi.

Athari: Kutokana na udhaifu ulioripotiwa na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, katika Udhibiti wa Ndani na Utawala bora katika Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Idara, Ofisi za Balozi, Wakalana Taasisi nyingine umechangia kuongezeka kwa taasisi zilizopata Hati yenye Mashaka na Hati Mbaya. Kutokuwepo kwa Kamati ya Ukaguzi na Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani kunachangia kuongezeka kwa matumizi mabaya ya rasilimali za umma, kuongezeka kwa udhaifu uliogundulika kwenye mifumo ya makusanyo na usahihi wa taarifa za fedha na rasilimali. Pia, mapungufu katika Bodi za Ushauri za Wizara na taasisi nyingine za Serikali yanasababisha usimamizi dhaifu wa rasilimali za taasisi husika, utawala wa sheria na utawala bora.

Pendekezo:

i. Serikali ifikirie kuja na Sheria na kanuni zitakazosimamia shughuli za ukaguzi wa ndani kama ilivyo kwa sheria Namba 11 ya mwaka 2008 ambayo inamhusu mkaguzi wa nje. Kuwepo kwa sheria hii kutamuongezea Mkaguzi wa Ndani ufanisi kwa kuwa na mtiririko muafaka wa utendaji, kuripoti, upatikanaji wa rasilimali na usimamizi wa kitengo hiki.

ii. Wakati mchakato wa upatikanaji wa sheria unaendelea, Mkaguzi Mkuu wa Ndani (IAG) kwa kushirikiana na Mlipaji Mkuu wa Serikali watoe waraka utakaotoa maelekezo ya muundo wa Kamati za Ukaguzi wa Ndani utakaojumuisha idadi kubwa zaidi ya wajumbe kutoka nje ya taasisi husika tofauti na ilivyo sasa, pamoja na mtiririko wa kuripoti utakaoongeza uwazi na uhuru kwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani na Kamati ya Ukaguzi.

Jambo la 6: Usimamizi wa Rasilimali Watu na Mishahara

Dosari ambazo zimeendelea kujitokeza katika usimamizi wa rasilimali watu na mishahara ni kama ifuatavyo:

- ✓ Kulipa mishahara kwa watumishi ambao hawapo kwenye utumishi wa Umma (watumishi hewa).
- ✓ Makato mbalimbali ya kisheria yaliyokatwa kwenye mishahara ya watumishi ambao sio watumishi wa Umma.
- ✓ Kuchelewa na kutokupeleka makato ya kisheria ya watumishi kwenye taasisi husika
- ✓ Watumishi kukaimu nafasi zaidi ya muda unaokubalika kisheria.
- ✓ Posho ya kukaimu nafasi mbalimbali kutokukatwa kodi
- ✓ Upungufu wa watumishi
- ✓ Baadhi ya taasisi kushindwa kufanya tathmini na kupima utendaji wa watumishi
- ✓ Dosari katika utunzaji wa kumbukumbu za watumishi
- ✓ Kutokulipa stahiki mbalimbali za watumishi.

Athari: Mapungufu katika usimamizi wa rasilimali watu yanaathiri ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya serikali. Hivyo, kupelekea kuzorota kwa utoaji huduma kwa wananachi.

Pendekezo:

i. WAJIBU inapenda kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi shupavu wa Rais Dr. John Pombe Magufuli kwa kulishughulikia kwa nguvu zote tatizo la watumishi hewa na vyeti feki katika ajira ya Serikali.

ii. Mbali na jitihada zilizochukuliwa na Serikali, bado kuna umuhimu wa kuimarisha mifumo ya ndani ya usimamizi wa rasilimali watu ikiwa ni pamoja na:

- Kutathmini ubora na ufanisi wa mfumo wa LAWSON katika kudhibiti watumishi hewa,
- Kutoa madaraka katika ngazi za chini za utawala katika kusimamia utekelezaji wa mfumo wa udhibiti wa rasilimali watu serikalini,
- Serikali kuwawajibisha Maofisa wote wa Serikali watakao sababisha uwepo wa watumishi hewa, na
- Serikali ifuatilie kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo ililipwa makato yaliyotokana na malipo ya mishahara hewa.

Jambo la 7: Upungufu wa Watumishi

Kumekuwa na tatizo la muda mrefu la uhaba wa wafanyakazi katika ofisi za serikali. Katika sampuli ya taasisi zilizokaguliwa thelathini na nane, nafasi 11,892 zilikuwa wazi ikilinganishwa na mahitaji ya watumishi 24,568 katika Wizara, Sekretariati za Mikoa Idara, Wakala pamoja na Taasisi zingine. Upungufu huu ni asilimia 48 ya mahitaji ya watumishi.

Tatizo hili limejitokeza kwa kiasi kikubwa katika wizara na sekretatieti za mikoa. Tatizo la uhaba wa wafanyakazi kwa Wizara 3 na Sekretarieti za mikoa 15 zilizoongoza ni kama inavyoonekana katika Kielelezo Na 5 hapo chini.

Kielelezo Na. 5: Wizara na Sekretarieti za Mikoa Zinazoongoza kwa Uhaba wa Watumishi



Athari: Upungufu wa watumishi wa umma unaathiri utendaji wa Serikali na kusababisha kutokufikia malengo yaliyokusudiwa kwa kukosa mchango wa taaluma mbalimbali katika utekelezaji wa mipango mingi ya Serikali. Aidha, mgawanyo wa majukumu na uhamisho wa watumishi ambavyo ni muhimu katika mfumo wa udhibiti wa ndani hauwezi kufanyika kwa ufanisi panapokuwa na uhaba mkubwa wa watumishi.

Pendekezo: Serikali inashauriwa ifanye tathmini ya kina kuhusu mahitaji halisi ya watumishi kabla hata haijafikiria kuongeza wafanyakazi hao. Tathmini hii ihusishe uchambuzi wa miundo ya taasisi za Pendekezo Serikali, muingiliano wa kazi kati ya taasisi moja na nyingine ya Serikali, taasisi ambazo zingeweza kuunganishwa na kuleta ufanisi mkubwa zaidi na upunguzaji wa gharama za uendeshaji.

Jambo la 8: Utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma 2011

Manunuzi ya umma yanatumia kiasi kikubwa cha rasilimali za Serikali ili kutekeleza shughuli zilizopangwa. Inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya matumizi ya serikali yanagharamia manunuzi ya mali au huduma zinazohitajika na serikali. Katika ukaguzi wa Wizara na taasisi mbalimbali za serikali, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alibaini mapungufu hasa katika utaratibu wa utoaji wa zabuni, utekelezaji na usimamizi wa mikataba na manunuzi ambayo hayakufanyika kwa kuzingatia matakwa ya sheria na kanuni zake. Kwa kipindi cha mwaka 2015/16 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aligundua mapungufu yafuatayo kwenye manunuzi na usimamizi wa Mikataba;

- Malipo yasiyoambatana na risiti za Kielektoniki,
- Malipo bila kukata kodi ya zuio,
- Malipo yasiyokuwa na viambatisho,
- Masurufu yasiyorejeshwa,
- Manunuzi yaliyofanyika nje ya mpango wa manunuzi,
- Matangazo katika Miundombinu bila Mikataba,
- Ununuzi kupitia chanzo kimoja,
- Matumizi yasiyo ya lazima,
- Ununuzi wa boti ambao haujathibitishwa,
- Ununuzi wa vifaa kutoka kwa Wazabuni wasioidhinishwa, na
- Mkataba usiotekelezwa.

Athari: Kiasi kikubwa cha rasilimali za Umma kina potea kutokana na Ubadhirifu unaofanyika kupitia njia za manunuzi. Pia, Serikali inashindwa kutoa huduma za jamii kutokana na gharama kubwa za manunuzi ya umma zinazosababishwa na kutokuzingatiwa kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma 2011.



Pendekezo:

i. Serikali ichukue hatua kali za kisheria kwa wahusika wote walioshindwa kufuata na kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2013.

ii. Serikali ipitie Sheria ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 ili kuiboresha na kuziba mianya ya ubadhirifu unaofanyika.

Jambo la 9: Ukaguzi wa Vyama vya Siasa

Katika vyama vya siasa kumekuwa na uandaaji duni wa vitabu vya msingi vya fedha kama vile mizania ya majaribio, vitabu vya fedha taslimu, vitabu vya kila akaunti na vitabu vikuu ambavyo hutoa taarifa za kuaminika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha. Pia, taarifa nyingi za fedha hazikuwa na nyaraka, jambo ambalo lilipunguza uwezo wa mkaguzi kukagua hesabu kwa usahihi na uwazi. Baadhi ya masuala yaliyobainika katika ukaguzi wa vyama vya siasa ni pamoja na yafuatayo:

a) Vyama vinne (4) vyenye usajili wa kudumu kati ya kumi na tisa (19) vilivyokaguliwa havikuwasilisha taarifa za fedha za kila mwaka kama inavyoelekezwa na sheria. Vyama hivyo ni National Reconstruction Party (NRA), United People's Democratic Party (UPDP)), Party for People's Redemption (CHAUMMA) na Union for Multiparty Democracy (UMD).

b) Kuhusu usimamizi wa rasilimali watu na mishahara, ilibainika kuwa mbali na Makatibu Wakuu ambao hujitolea, waajiriwa wengine wa Vyama vya Siasa hawana mikataba yenye nguvu za kisheria zinazoeleza majukumu, uwajibikaji na malipo yao.

Athari:

i. Kutokuwasilishwa kwa taarifa za fedha na baadhi ya vyama vya siasa kunatia mashaka juu ya matumizi yaliyofanyika kwenye vyama hivyo. Hali hii ni dalili mbaya ya uwajibikaji na usimamizi wa fedha za umma unaotakiwa kuanzia katika vyama vya siasa ambako ndipo viongozi wa Serikali wanaanza kulelewa.

ii. Kama vyama vya siasa vina watumishi ambao hawana mikataba na ajira rasmi, hii inaweza kupelekea taifa kupata viongozi ambao hawajapekuliwa vizuri. Kama Taifa halitakuwa makini, kuna hatari ya kupata viongozi wasio waadilifu na hata wasio wa Tanzania halali.

Pendekezo:

i. Ili kuongeza uwazi, uwasilishaji na ulinganisho wa ufanisi wa Vyama vya Siasa, vyama vinapaswa kuandaa taarifa za fedha kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu. Utumiaji wa mfumo unaofanana katika kuandaa hesabu za vyama utasababisha kufanana katika kuandika miamala na kuandaa taarifa za fedha za vyama vya siasa.

ii. Msajili wa Vyama vya Siasa aandae utaratibu utakaowezesha kuvijengea uwezo Vyama vya Siasa kuandaa taarifa za fedha kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu.

iii. Msajili wa Vyama vya Siasa asisitize kuwa, pamoja na masharti mengine, akaunti ya benki iwe ni mojawapo ya masharti ya kusajiliwa kwa chama cha siasa.

Jambo la 10: Ukaguzi Maalum wa Fedha za Gavi Alliance kwa Ajili ya Chanjo ya Surua Rubella

Wizara ya Fedha na Mipango ilipokea jumla ya Shilingi 20.9 billioni sawa na (USD 12,791,693) kutoka GAVI Alliance, na kiasi hicho chote kilipelekwa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ajili ya zoezi la chanjo ya Surua Rubella. Kati ya kiasi hicho, Shilingi Bilioni 1.00 zilitengwa kwaajili ya gharama za uendeshaji na Shilingi bilioni 19.10 zilitolewa kwa ajili ya kufanikisha zoezi la chanjo.

Katika ukaguzi uliofanywa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alibaini ni asilimia 61 tu ndiyo zilitumika kutoa chanjo ya surua.

Athari: Asilimia 39 ya fedha za mradi huu hazikutumika moja kwa moja katika utoaji wa chanjo ya Surua Rubella kama ilivyokusudiwa. Hali hii, ilipelekea watoto wengi kukosa chanjo ya surua kama ilivyokusidiwa kwenye mradi huu.

Pendekezo: Serikali iwachukulie hatua kali wote waliohusika na ubadhirifu wa fedha za mradi huu ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani kwa madhumuni ya kuzirejesha fedha zilizoibiwa.

Hitimisho:

WAJIBU inaamini kuwa kwa taasisi zinazohusika na uwajibikaji pamoja na wananchi wakizielewa vizuri ripoti za CAG, itachangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza uwajibikaji na utawala bora hapa nchini.

Kuna umuhimu kwa Serikali na wadau wengine wote wakijumuishwa Wananchi kuhakikisha kuwa mapungufu na mapendekezo yaliyotolewa na CAG yanafanyiwa kazi kikamilifu. Hii itaongeza ufanisi wa shughuli za Serikali Kuu na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo ya nchi na hatimaye mwananchi mmoja mmoja.

WAJIBU inategemea itakuwa rahisi kwa wananchi wa kawaida kusoma na kulielewa chapisho hili na mengine ya ripoti ya CAG ya ukaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma ambayo yametengenezwa na kusambazwa na WAJIBU kwa kushirikiana na wadau wengine kama GIZ.

WAJIBU itashukuru sana kupata mrejesho kutoka kwa wasomaji wa chapisho hili kuhusu namna ya kuliboresha na kulifanya liweze kufaidisha wasomaji wengi zaidi nchi nzima.

WAJIBU - Institute of Public Accountability

P. O. Box 13486 Dar Es Salaam

Barua pepe: admin@wajibu.or.tz ; Simu: +255 22 266 6916

Tovuti: www.wajibu.or.tz